SALT LAKE COUNTY
AGING & ADULT SERVICES

# MIPANGO NA HUDUMA

(385) 468 - 3200
slco.org/aging

**Mpango wa Msaada kwa Watunzaji** hutoa taarifa na usaidizi, mafunzo ya bure, matukio, vikundi vya misaada, na ushauri kwa watunzaji wote wa familia na jamii zisizo rasmi. Watunzaji wasiolipwa wanaweza pia kutuma maombi ya huduma za mapumziko ya muda mfupi.

**Mpango wa Msaada wa Uzeeni** hutoa huduma za kusimamia matibabu na huduma za nyumbani kwa watu wanaokidhi mahitaji ya umri/mapato na wanaotaka kuendelea kuzeeka wakiwa nyumbani kwao.

**Mababu na Mabibi wa Kulea** hujitolea kuwalea watoto walio hatarini katika mazingira mbalimbali ya Wilaya ya Salt Lake.

**Mpango wa Ukuzaji wa Afya na Elimu** hutoa mafunzo yanayozingatia ithibati ili kuwawezesha washiriki kuendelea kufanya shughuli mbalimbali kwa miili yao, kudhibiti hali zao sugu, kuepuka kuanguka na kuendelea kujiunga na jamii.

**Mpango wa Mashirikiano Makazi** hushughulikia wazee wasio na makazi au wanaohitaji nyumba za wazee za bei nafuu, za watu wenye kipato cha chini na wanaotatizika kutuma maombi ya makazi.

**Mpango wa Meals on Wheels** hutoa chakula moto cha mchana kwa watu wazima walio na umri wa miaka 60 na zaidi wasioweza kutoka nyumbani.

Mpango wa Huduma kwa Wanaozeeka na Watu Wazima wa **Mchunguzi Maalum** husaidia na kulinda haki za watu wanaoishi katika vituo vya utunzaji wa muda mrefu.

**Mpango wa Kuwasaidia Wanajamii** hujibu maswali kuhusu masuala yanayohusiana na kuzeeka, huwasaidia watu binafsi kujiandikisha ili wapate huduma, huwaelekeza watu kwa watoa huduma wengine, na husaidia watu kujiandikisha, kujibu maswali na kutatua matatizo ya **Mpango wa Bima wa Afya ya Wazee (SHIP) na Medicare**.

**Mpango wa Wakimbizi** hutoa huduma za utetezi, rasilimali, na ushirikiano wa kijamii kwa wakimbizi wazee wanaoishi katika Wilaya ya Salt Lake.

Mpango wa **Rides for Wellness** hutoa huduma za usafiri kwa watu wazima wenye umri wa miaka 60 au zaidi wasio na njia nyingine yoyote ya kusafiri kwenda kuhudhuria miadi muhimu ya matibabu ikiwa ni pamoja na huduma za dialisisi, tibakemikali, na nyingine.

**Vituo vya Wazee** vya Wilaya ya Salt Lake hutoa fursa za kujifunza, kujumuika, kufanya kazi za kujitolea, kujihusisha na jamii, na ustawi kwa washiriki. Vituo vya Wazee vinawakaribisha watu wenye umri wa miaka 60 au zaidi.

**Mpango wa Wenzi wa Wazee** hushirikiana na wafanyakazi wa kujitolea ili kusaidia wazee dhaifu na waliotengwa na kuzeeka wakiwa nyumbani badala ya mahali pa utunzaji wa muda mrefu.

Mpango wa Huduma kwa Wanaozeeka na Watu Wazima hufanya mkataba na **Kituo cha Sheria cha Wazee cha Huduma za Kisheria cha Utah** kwa ajili ya kutoa misaada ya kisheria kwa wazee wenye umri wa miaka 60 na zaidi wanaoishi katika Wilaya ya Salt Lake. Piga simu kwa (801) 328 - 8891 ili upate usaidizi.

**Huduma kwa Wanajeshi Wastaafu Katika Makazi na Jamii**husaidia wanajeshi wastaafu wanaotaka kubaki nyumbani kwao, lakini wanahitaji huduma stadi za utunzaji wakiwa nyumbani, usimamizi wa matibabu, na msaada wa kufanya shughuli za maisha ya kila siku.

**Fursa za Kujitolea** huwapa watu wa rika zote nafasi ya kuleta mabadiliko katika jamii yetu. Toa msaada kwa Kituo cha Wazee, wasilisha chakula kupitia mpango wa Meals on Wheels, kuwa rafiki ya mzee aliyetengwa, na zaidi.